

SHULE YA SEKONDARI MUKWASA,  
S. L. P 04,  
HAI.  
SIM: 0788-414550  
15/12/2020.

KUMB. Na. MUK/SS/2122/RGFI/VOL.01/2021

JINA LA MWANAFUNZI: .....

S. L. P .....

.....

YAH: MAAGI ZO YA KUJI UNGA NA SHULE YA SEKONDARI MUKWASA WILAYA YA HAI  
MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021.

1.0 Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari MUKWASA ipo katika Kijiji cha MUNGUSHI Kata ya MASAMA KUSINI, umbali wa Kilomita SITA (km 6), Kaskazini mwa Halmashauri ya Hai.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza rasmi tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia.

2.1 Sare za Shule ni rangi nyeusi

(a) Wasichana

- Sketi mbili (2) za marinda box ambazo zinavuka magoti – utaonyesha siku ya kuripoti
- Mashati meupe mawili (2) ya mikono mifupi aina ya Tomato (yawe mapya kulingana na ukubwa wa mwanafunzi).
- Sweta moja (1) linalofanana na rangi ya sketi
- Soksi jozi mbili (2) nyeupe
- Viatu vyeusi vya kamba viwe vya ngozi vinavyoweza kupigwa kiwi na visiwe na visigino virefu.
- Huruhusiwi kusuka nywele wala kunyoa kipara au staili mfano kiduku, panki n.k

NB: *Rangi ya hijabu ifanane na rangi ya shati (iwe nyeupe)*

(b) Wavulana

- Suruali mbili (2) ndefu ambazo hazibani, upana wa chini usizidi inchi 16-18.
- Mashati mawili (2) aina ya Tomato
- Sweta moja (1) inayofanana na rangi ya suruali
- Soksi jozi mbili (2) nyeupe
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vinavyoweza kupigwa kiwi na visiwe na kisigino kirefu.
- Mkanda wa suruali mweusi usio na madoido
- Mwanafunzi atakaye vaa modo au kata kei ataadhibiwa na suruali itakatwa
- Huruhusiwi kunyoa kipara wala staili mfano kiduku, panki n.k

NB: *Angalia kitambaa kilicho ambatanishwa*

## 2.2 Sare ya michezo kwa shule hii ni

- i. Wavulana: Tracksuit ya rangi nyeusi
  - ii. Wasichana: Tracksuit ya rangi nyeusi.
- Sare hizi zitakaguliwa siku ya kuandikishwa mwanafunzi.

## 2.3 CHAKULA:-

Kuna kamati ya wazazi inayohusika na chakula cha wanafunzi, mzazi/mlezi fika shulenii watakujulisha namna ya kuchangia.

## 2.4 PICTA SITA ZA PASSPORT SIZE:

Na faili moja (folder file) lisiwe la plastiki kwa ajili ya kumbukumbu

## 2.5 MAZINGIRA:

- i. Kila mwanafunzi aje na mti mmoja wa kivuli au matunda wa kupanda katika eneo la shule.
- ii. Uje na fagio la chelewa kwa ajili ya usafi na mazingira ya shule pamoja na fyekeo na ndoo ndogo ya ujazo wa lita kumi.

## 3.0 VIFAA VYA DARASANI

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na vifaa vya darasani kwa ajili ya masomo na mazoezi ya kitaaluma hapa shuleni kama ifuatavyo:-

- (i) Madaftari ya masomo 10 (Counter book Quire 3)
- (ii) Daftari ndogo 10 kwa ajili ya mazoezi
- (iii) Mathematical set (Mkebe wa vifaa vya hisabati)
- (iv) Kalamu ya wino (Bluu au Nyeusi), Penseli, Kifutio na Rula ndefu.
- (v) Dictionary (OXFORD) English to English
- (vi) Mathematical table (4-figure)
- (vii) Begi la kubebia madaftari na vitabu.

## 4.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII .

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 5 ya mwaka 1978 na kama iliyvorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Mafunzo ya Ufundu yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

### 4.1 (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation)

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyininge utakazopewa

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

(g) Kuvala sare ya shule wakati wote unapotakiwa

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

(i) Kutunza mali za umma

- 4.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule au kusimamishwa masomo
- a. Uasherati, ushoga na usagaji
  - b. Ubakaji
  - c. Wizi
  - d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, ugoro na kadhalika
  - e. Kupigana au kupiga
  - f. Kuharibu kwa makusudi mali za umma, kama vile: kuandika katika kuta za majengo ya shule, kuhaniblu meza na viti kwa michoro na maandishi yasiyo na msingi, kuvunja vioo, mabomba n.k
  - g. Kudharau bendera ya Taifa
  - h. Kupata mimba/kusababisha mimba
  - i. Kuoa au kuolewa
  - j. Kutoa mimba/kushiriki kutoa mimba
  - k. Kukataa adhabu kwa makusudi
  - l. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo
  - m. Kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
  - n. Kumiliki, kukutwa, kutumia simu ya mkononi au laini ya simu (sim card) katika mazingira ya shule
  - o. Kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa
  - p. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kwa kunywa sumu n.k
  - q. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
  - r. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
  - s. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako, walimu/walezi kwa ujumla
  - t. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa.

4.3 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shulenii na wanafunzi.

- a. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Form hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shulenii.
- b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARI BU SANA KATIKA SHULE HII  
KIULA P. E

MKUU WA SHULE



15/12/2020

**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**  
**SHULE YA SEKONDARI MUKWASA**  
**S.L.P 04, HAI**

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

(Taarifa hii ijazwe na wanafunzi wote wa kidato cha kwanza na wanafunzi wanaohamia katika shule hii)

JINA LA KWANZA .....

TAREHE YA KUZALIWA .....

KABILA ..... URAIA .....

DINI ..... DHEHEBU .....

JINA LA BABA ..... HAI/AMEFARIKI

JINA LA MAMA ..... HAI/AMEFARIKI

JINA KAMILI LA MLEZI (KAMA HANA WAZAZI) .....

UHUSIANO NA MLEZI .....

KAZI YA BABA/MAMA/MLEZI .....

JAMAA KATIKA FAMILIA

- i. IDADI YA KAKA .....
- ii. IDADI YA DADA .....
- iii. YEYE NI WANGAPI KATIKA FAMILIA .....

ANUANI YA NYUMBANI .....

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI .....

ULEMAVU WOWOTE WA VIUNGO/AKILI .....

**NB: Ambatanisha cheti cha kuzaliwa**

**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**  
**SHULE YA SEKONDARI MUKWASA**  
**S.L.P 04, HAI**

**HATI YA UTII WA SHERIA**

**A: MWANAFUNZI**

JINA LA MWANAFUNZI .....  
TAREHE YA KUZALIWA .....  
JINA MZAZI/MLEZI .....  
UHUSIANO WA MLEZI (BABA, MJOMBA, KAKA N.K) .....  
KAZI YA MZAZI/MLEZI .....

Mimi ..... Nikiwa mwanafunzi wa shule hii, nakubali kuwa, umma wa nchi hii ya Tanzania ndiyo uliyonipa nafasi hii maalumu ya masomo, ili nimalizapo niweze kuitumikia nchi katika kuleta maendeleo. Hivyo basi ninaahidi kwamba, nitajibidisha hapa shulenii na pia nimalizapo shule. Ili kutimiza shabaha hiyo na ninakubali na kuahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitatii sheria za shule na amri nitakazopewa na uongozi wa shule (walimu na serikali ya wanafunzi). Nikiwa na malalamiko au maoni nitayafikisha kwa uongozi wa shule kufuatana na utaratibu uliowekwa bila kuogopa chochote.

Tarehe ..... Saini .....

**B: MZAZI/MLEZI**

Mimi Bwana/Bibi ..... Mzazi/Mlezi wa .....  
Nimesoma kwa makini sheria za shule kama zilivyoandikwa katika maagizo kwa wazazi na nazikubali sheria hizo na nitashirikiana na shule kuona kuwa mwanangu anazingatia kwa makini kwa manufaa ya Umma.

Tarehe ..... Saini ..... Namba ya simu .....

**PRESIDENT'S OFFICE**  
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**  
**REQUEST OR MEDICAL EXAMINATION FORM**

To the Medical officer

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
Please examine (*name of student*) ..... who has been selected to join this school or his fitness as a student in the following areas.

1. Eye sight .....
2. Hearing .....
3. Stool .....
4. Urine .....
5. Blood .....
6. Asthma/Tuberculosis .....
7. Pregnancy .....
8. Other diseases .....

**MEDICAL CERTIFICATE (To be completed by a medical officer)**

I have examined the above and consider that he/she is physically fit as a student.

NAME(medical officer) ..... SIGNATURE .....

STATION ..... DESIGNATION .....

DATE: .....